JAMHURI YA KENYA

WIZARA YA ELIMU

HATI YA UTOAJI HUDUMA KWA UMMA

NAMBARI	HUDUMA	KINACHOHITAJIKA	GHARAMA YA HUDUMA (ikiwa inahitajika)	MUDA
1	Kujibu barua	Ombi lililoandikwa	Hakuna Malipo	Siku 14 za Kikazi
2	Usajili wa shule za upili za umma na binafsi na vyuo vya stashahada	Barua ya maombi: Kumbukumbu za kikao cha Halmashauri ya Elimu kwenye Gatuzi (Kaunti na Kaunti ndogo), Taarifa za kuthibitisha viwango na utathmini wa viwango: Ripoti ya hali ya afya ya umma; Nakala ya cheti cha umiliki wa ardhi au kukodisha ardhi; Mchoro wa shule; Rekodi za viwango vya elimu vya walimu.	Shule za Upili za Umma na vyuo –usajili wa muda wa mwaka mmoja, miaka mitano au wa kudumu, ada ni shilingi 2,000 kila kiwango; Shule za upili za kibinafsi na vyuo- usajili wa muda wa mwaka mmoja, miaka mitano au wa kudumu,ada ni shilingi 10,000 kila kiwango	Siku 21 za Kikazi
3	Usambazaji wa hazina ya kufadhili mpango wa utoaji wa elimu ya msingi na ya shule za upili za kutwa bila malipo	Cheti cha kusajiliwa kwa shule, Taarifa sahihi kuhusu idadi ya wanafunzi shuleni kama ilivyonakiliwa kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Elimu (NEMIS); Nambari sahihi za akaunti za shule za benki na Jina la benki	Hakuna Malipo	Siku 7 za Kikazi baada ya kupokea fedha kutoka kwa Hazina kuu ya Serikali
4	Uteuzi na usajili wa wanafunzi wa stashahada kwenye mafunzo ya walimu wa shule za msingi (DPTE)	Kusajiliwa kwenye maeneo (Kaunti ndogo), awe na alama ya C wastani au zaidi kwa wanafunzi wa kawaida na alama ya C-Hasi kwa wanafunzi walio na ulemavu	Hakuna Malipo	Siku 40 za Kikazi
5	Uteuzi na usajili wa wanafunzi wa stashahada kwenye mafunzo ya walimu wa shule za chekechea (DECTE)	Kusajiliwa kwenye maeneo (Kaunti ndogo); Alama ya chini zaidi kwenye Mtihani wa kuhitimu wa Shule za Upili (KCSE), iwe C Wastani au alama sawia (kuambatana na viwango vya Baraza la Kitaifa la Mitihani (KNEC). Wanafunzi walio na ulemavu watasajiliwa ikiwa wana alama ya C - Hasi kwenye Mtihani wa Kuhitimu wa Shule za Upili (KCSE) au kiwango sawia.	Hakuna Malipo	Siku 40 za Kikazi
6	Uteuzi na usajili wa wanafunzi wa stashahada kwenye mafunzo ya elimu ya wanafunzi walio na mahitaji maalum (SNE)	Lazima awe; Umri wa chini ya miaka 50; Awe amehudumu kama mwalimu katika Tume ya Huduma kwa Walimu (TSC) kwa kipindi cha miaka mitano, awe na cheti cha P1 au amepandishwa cheo adi P2 kupitia mafunzo ya utendakazi; awe raia wa Kenya	Hakuna Malipo	Siku 30 za Kikazi
7	Uteuzi na usajili wa wanafunzi katika shule za upili za umma	Matokeo ya Mtihani wa Darasa la Nane (KCPE) wa mwaka uliotangulia	Hakuna Malipo	Siku 21 baada ya kutangazwa kwa matokeo ya Mtihani wa Darasa la Nane, (KCPE)
8	Uteuzi wa Halmashauri za Usimamizi katika Taasisi za masomo ya msingi.	Orodha za walioteuliwa na Kumbukumbu za mikutano, Wasifukazi wa walioteuliwa; Kumbukumbu za Vikao vya Uteuzi, Kumbukumbu za Mikutano ya Halmashauri ya Elimu kwenye Gatuzi (Kaunti)	Hakuna Malipo	Siku 30 za Kikazi
9	Usambazaji wa ufadhili wa Miundomsingi na vifaa vya maabara kwa shule za upili za umma	Orodha ya shule zilizopendekezwa kutoka kwa Halmashauri ya Elimu kwenye Gatuzi (Kaunti) (CEB) au barua maalum ya maombi	Hakuna Malipo	Siku 30 za Kikazi
10	Uidhinishaji wa vyeti vya elimu	Vyeti asili na stakabadhi za kuthibitisha; Nakala zilizoidhinishwa za vyeti asilia zilizopigwa muhuri pande zote mbili na taasisi zilizotoa	Hakuna Malipo	Siku 1 ya Kikazi
11	Usajili wa wanafunzi katika vituo vya masomo kwa watu wazima na wanaoendelea na masomo hayo (ACE)	Sajili ya waliosajiliwa	Hakuna Malipo	Siku 7 za Kikazi
12	Utoaji wa vyeti kwa wanafunzi wa elimu ya watu wazima	Ombi lililoandikwa	Hakuna Malipo	Siku 7 za Kikazi
13	Utoaji ufadhili wa kimasomo	Kujaza fomu ya Maombi ya ufadhili unapotangazwa; kuhudhuria vikao vya usaili unapoorodheshwa	Hakuna Malipo	Siku 60 za Kikazi
14	Kuidhinisha wanafunzi wanaoenda kwa mafunzo/masomo katika mataifa ya nje	Vyeti vya Idhini, Cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha taifa (ID) Kitambulisho cha mdhamini Picha ndogo ya Mwanafunzi, Barua ya idhini ya Halmashauri ya utoaji mikopo ya elimu ya juu (HELB) kwa wanaoenda kwa masomo ya uzamili	Hakuna Malipo	Siku 1 ya Kikazi
15	Utoaji habari sahihi na muhimu kuhusu, Sayansi,Teknolojia na Uzinduzi	Ombi lilioandikwa	Hakuna Malipo	Siku 7 za Kikazi
16	Kutangaza, kusambaza mawasiliano kuhusu sayansi, utafiti na teknolojia, Tuzo na Ufadhili	Tangazo, Ombi lililoandikwa	Hakuna Malipo	Siku 7 za Kikazi
17	Uteuzi wa Halmashauri za Usimamizi kwenye vyuo vya mafunzo Anuwai	Orodha ya walioteuliwa, tawasifu za walioteuliwa, Kumbukumbu za mikutano ya vikao vya uteuzi	Hakuna Malipo	Siku 90 za Kikazi

TUMEJITOLEA KUTOA HUDUMA BORA KWA HESHIMA

Habari kuhusu huduma zozote au bidhaa ambazo haziambatani na viwango vilivyoorodheshwa au afisa yeyote ambaye hatazingatia utoaji huduma bora kwa heshima zinaweza kutolewa kwa:

Waziri,
Wizara ya Elimu,
Jumba la Jogoo "B" Barabara yaTaifa,
S.L.P 300400-00100
Simu: +254(0)02033185/3318585
Barua Pepe: info@education.go.ke

Katibu wa Tume/Afisa Mkuu Mtendaji,
Tume ya Utekelezaji Haki, Orofa ya Pili,
Jumba la West End Towers, Barabara ya Waiyaki , Nairobi.
S.L.P 20414-00200 Nairobi
Simu: +254(0)202270000/2303000
Barua Pepe: complain@ombudsman.go.ke